# Mabucha 17 yabainika kuendeshwa kinyemela

**Kahama**
**SALVATORY NTANDU**

BODI ya Nyama Tanzania kwa kushirikiana na maofisa biashara wa Manispaa ya Kahama, Mkoani Shinyanga, wamefanya ukaguzi wa maduka ya nyama 61 ambapo wamebaini maduka 17 wamiliki wake hawana leseni za biashara.

Hayo yalibainisha juzi na Ofisa Usajili wa Bodi ya Nyama Tanzania, Kakuru Sostenes, kwenye kikao kazi kilichowakutanisha wamiliki wa maduka na wafanyabiashara wa nyama wilayani hapa.

Alisema ukaguzi huo umebaini maduka mengi kutokidhi vigezo vya kutoa huduma hiyo huku baadhi ya wamiliki wake kutokuwa na leseni za biashara kutoka idara za manispaa zinazowatambulisha kisheria.

"Tumebaini wengi wenu hamna leseni za biashara, maduka yana mizani mbovu, sehemu za biashara mazingira yake machafu, matumizi ya magogo kukatia nyama bado yanaendelea na hakuna majokofu ya kuhifadhia nyama," Sostenes, alisema.

Alifafanua kuwa bodi hiyo haitotoa usajili kwa duka lolote likalobainika kutokidhi vigezo vya kisheria ikiwemo leseni za biashara na kuwataka wafanyabiashara hao kuzingatia takwa hilo muhimu kabla ya kuanza kutoa huduma ya kuuza nyama na kuepuka kufungiwa biashara zao.

Kwa upande wake, Ofisa Biashara wa Manispaa hiyo, Cryirina Kirenga, alisema baada ya ukaguzi kukamilika wafanyabiashara hao walilazimika kusitisha biashara hiyo kwa ajili ya kulipia gharama za usajili ili waweze kupata vibali vitakavyowaruhusu kutoa huduma hiyo.

"Tumewapa maelekezo ya namna ya kurasimisha biashara hii na wote wamekubali kulipia gharama za usajili wa biashara zao, pia bodi ya nyama imeanza kuwasajili katika mfumo maalum ili waweze kuwafuatilia kwa ukaribu," Kirenga, alieleza.

Kufutia kuibuka kwa hoja hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akalazimika kutoa siku 14 kwa wafanyabiashara hao kuhakikisha wanarasimisha biashara hiyo kwa kufanya sajili na watakoshindwa watafungia kutoa huduma hiyo.

"Haiwezekani turuhusu biashara holela ya nyama Kahama, kitengo cha biashara na watu wa afya piteni fanyeni ukaguzi ili kuwabaini wafanyabiashara wanaoiibia serikali mapato na wanaowalisha watu nyama ambazo hajafanyiwa ukaguzi," Macha, alieleza.

Zaidi ya maduka 61 yamefanyiwa ukaguzi na bodi hiyo na kuanza kuyasajili kwa mfumo maalum ili kuweza kuwafuatilia kwa ukaribu zaidi na kutoa muda wa miezi sita ya matazamio ili kuwabaini ambao hawatazingatia sheria na taratibu za afya.

**Ofisa Biashara**

Tumewapa maelekezo ya namna ya kurasimisha biashara hii na wote wamekubali kulipia gharama za usajili wa biashara zao, pia bodi ya nyama imeanza kuwasajili katika mfumo maalum ili waweze kuwafuatilia kwa ukaribu...

Scanned with CamScanner

majuriko pamoja na ujali za barabarani iliyofanyika leo katika Kijiji cha Champumba, Wilayani Chamwino Mkoani Dodoma.

# Jafo aipa machinjio ya kizota kujenga mfumo wa kutibu majitaka

NA DOTTO KWILASA DODOMA.

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Selemani Jafo ameupa uongozi wa machinjio ya kisasa ya Kizota jijini Dodoma miezi sita kurekebisha changamoto ya utiririshaji wa majitaka ovyo.

Waziri Jafo ametoa agizo hilo jana jijini hapa alipofanya ziara ya kikazi katika machinjo hiyo kwa ajili ya kukagua udhibiti wa majitaka na utunzaji wa mazingira kwa ujumla.

Alisema kuwa kila kiwanda lazima kiwe na mpango wa namna ya kuyatibu majitaka na kudhibiti utiririshaji wake kuepusha yasiende kwenye makazi ya watu na kusababisha madhara kiafya.

"Nafahamu machinjio hii ni miongoni mwa machinjo kubwa na ina soko kubwa katika nchi za Mashariki ya Kati wananunua nyama nami nimekuja hapa kujiridhisha kuhusu suala zima la utiririshaji wa majitaka," alisema na kuongeza;

Pamoja na kazi nzuri mnayofanya,nikiri wazi sijaridhishwa na hali ya usafi wa mazingira,hatuwezi kufanya kazi kwenye mazingira yanayohatarisha afya,jaribuni kuliangalia suala hili kwa umakini zaidi"alisema

Aidha alitumia nafasi hiyo kumuelekeza Meneja wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC) Kanda ya Kati Flanklin Rwezimula kufuatilia kazi ya kuhakikisha machinjio hiyo inatengeneza mfumo wa kutibu majitaka haraka.

Scanned with CamScanner

# Wavuvi hatarini kupata magonjwa mlipuko

**Na Grace Mwakalinga**, KYELA

WAVUVI na wafanyabiashara wa samaki kwenye mwalo wa Kafyofyo ulioko Ziwa Nyasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, wako hatarini kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na kutokuwa na vyoo.

Kutokana na hali hiyo, wananchi hao wanalazimika kujisaidia vichakani hali ambayo inasababisha vinyesi kusombwa na maji ya mvua na kuchanganyika kwenye mito na ziwa.

Hayo yalibainika juzi baada ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, timu ya wataalam wa afya na wakusanyaji wa mapato, kutembelea mwalo wa Kafyofyo kuangalia hali halisi ya eneo hilo.

Baada ya kujiridhisha kwamba hakuna vyoo na wakazi wa eneo hilo wakiwamo wavuvi na wafanyabiashara kujisaidia vichakani alitoa maelekezo kujenga vyoo vya muda wakati wakisubiri msimu wa mvua kumalizika na ushauri wa kitaalam kujenga vyoo bora vya kudumu.

Simon Josephat, mkazi wa Kijiji cha Kajunjumele, ambaye ni mchuuzi wa samaki na msanii wa kizazi kipya, alisema hali ya mwalo wa Kafyofyo si nzuri kutokana na kutokuwa na hakuna vyoo, hivyo kusababisha watu kujisaidia vichakani.

"Hali ya Kafyofyo si nzuri wananchi wanalazimika kujisaidia vichakani kwenye mito na ziwa kutokana na kukosekana na vyoo. Msimu huu wa mvua hata tukichimba vyoo vinabomoka kwa sababu ya mmomonyoko wa udongo," alisema Josephat.

Atupakisye Amon, mfanyabiashara eneo la Kafyofyo, alidai wameizoea hali hiyo ya kuendelea kujisaidia vichakani na kwamba baada ya mwenyekiti wa halmashauri na timu ya wataalam wa afya kuwatembelea kuwahamasisha kujenga angalau vyoo vya muda, wameanza utekelezaji.

Alisema mwalo wa Kafyofyo ni eneo ambalo linakusanya watu wa aina mbalimbali hivyo kukosekana kwa huduma ya vyoo kunahatarisha afya za wananchi.

Amon aliiomba serikali kuliangalia kwa jicho la pekee eneo hilo ambalo ni chanzo cha mapato kutokana na shughuli mbalimbali zinazofanyika ikiwamo uvuvi na biashara.

Pia alisema wananchi wahamasishwe kujenga vyoo bora vya kudumu na ikiwezekana serikali ijenge ili kukusanya fedha kwa watakaokuwa wanavitumia.

Aliongeza kuwa mwalo kwa Kafyofyo ni eneo ambalo wavuvi hawajajenga makazi ya kudumu kutokana na kazi yao kuwa ya kuhamahama.

Kingamkono alisema leo atapokea ripoti kutoka kwenye kamati ya fedha na mipango ili kubaini utekelezaji wa ujenzi wa vyoo vya muda kwenye mwalo wa Kafyofyo na namna ya kuondoa tatizo la ukosefu wa vyoo.

Scanned with CamScanner

# Fish farming proves beneficial for more than 11,000 people in various regions

By Guardian Correspondent, Morogoro

A TOTAL of 11,280 people from the country's various regions have benefited by modern fish farming training methods provided by Kongolwira Aquaculture Centre in Morogoro Region between 2010 and 2020.

This was revealed yesterday by the Acting Assistant Director of the Aquaculture Department in the Ministry of Livestock and Fisheries Dr Imani Kapinga about the centre's activities since it was established.

He said during the period the centre also produced 6,026,832 tilapia fish fingerlings that were distributed in Morogoro, Iringa, Coast, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Dodoma, Singida, Tabora, Unguja, Mwanza and Arusha regions.

"Part of the fingerlings were planted in natural dams in Morogoro, Coast, Singida and Iringa regions," he said.

Dr Kapinga said a total of 1,450 students from Sokoine University of agriculture (SUA), Universiry of Dar es Salaam (UDSM, University of Dodoma (Udom), Mbegani and Kunduchi Fish Colleges received practical training from the Kongolwira Aquaculture Centre.

He added that by working together with Tanzania Fisheries Research Institute (TAFIRI), SUA and UDSM, the Kinglolwira Centre has done various researches on fish farming.

The construction of the centre was done in four phases beginning 1979/1980 by digging 12 ponds of 200 sq metres each for fish farming.

However, the Phase 4 was completed in 2015 and 2017 by revamping of the hatching room and installation of jars for fingerling storage.

**He added that by working together with Tanzania Fisheries Research Institute (TAFIRI), SUA and UDSM, the Kinglolwira Centre has done various researches on fish farming**

Scanned with CamScanner